

MAAGIZO YA UBUNIFU – MASHUJAA

Mashujaa wa Imani, Sehemu ya 2

HADITHI YA SAMSONI

Watoto watafurahia kueleza hadithi ya Samsoni kupitia njia hii ya kusimua wakitumia sehemu tofauti za maisha yake.

VIFAA

- Ruwaza 1 ya ubunifu
- Rangi (krayoni, kalamu, na kadhalika.)
- Gundi
- Mrija unaotumika kunywa
- Pini ya kufunga karatasi
- Makasi



MAAGIZO

1. Kata ruwaza ya ubunifu katika mistari na kisha upake picha rangi.
2. Katikati ya kila karatasi duara, toboa shimo ndogo ili kuweka pini. Duara lililo kamili litakuwa upande wa chini na duara lililo na upande mmoja usiokuwepo litaenda upande wa juu ili kuona picha zilizoko upande wa chini.
3. Kata vipande vitatu kutoka kwa mrija. Kwa kutumia gundi, bandika kipande kimoja juu ya macho ya Samsoni, na vipande hivyo vingine viwili, vibandike juu ya jina Samsoni, katika duara la juu.
4. Kata macho ya ziada na jina "Samsoni" na uyabandike katika vipande vya mrija ili kuunda hali ya 3D. Sasa unaweza kukitumia kueleza hadithi ya Samsoni!

TAJI LA KIFALME

VIFAA

- Ruwaza ya taji kwa kila mtoto.
- Maumbo 4 makubwa ya almasi kwenye karatasi ya rangi.
- Maumbo 4 madogo ya almasi kwenye karatasi yenye rangi tofauti.
- Rangi (Krayoni, kalamu na kadhalika.)
- Gundi
- Utepe au uzi
- Mapambo ya johari



MAELEZO

1. Lipake taji rangi uzipendazo.
2. Kata ruwaza ya taji na kisha utoboe mashimo katika kila mwisho kwa ajili ya uzi.
3. Kwa kutumia gundi, pachika mapambo ya johari katika miviringo ya ncha za taji.
4. Bandika maumbo makumbwa ya almasi katikati ya ile mistari wima. Bandika maumbo madogo ya almasi juu ya maumbo makumbwa ili kuwakilisha johari katika taji.
5. Funga uzi au utepe katika mwisho wa taji na uzitumie kufunga taji juu ya kichwa cha mtoto.

Taji lipo tayari kuvaliwa. Unaweza kulitumia taji katika hadithi yoyote ya Mfalme Sauli, Daudi, au Sulemani.

YESU NDIYE NJIA (KIANGO CHA MLANGO)

Watoto watafurahia kupamba milango au sehemu yoyote ya nyumba yao kwa kutumia kiango hichi cha kusisimua.

VIFAA

- Ruwaza 1 ya kiango
- Mawingu 3 meupe ya karatasi nyeupe au karatasi povu
- Shina 2 za mti za karatasi za kahawia
- Vipande 2 vya sehemu ya juu vya mti vya karatasi ya majano
- Mawe 8 ya karatasi ya kahawia
- Rangi (Krayoni, kalamu, na kadhalika.)
- Mkasi
- Gundi

MAELEZO

1. Kata ruwaza ya kiango katika mstari wa nje. Usisahau kukata mviringo kutoka sehemu ya juu.
2. Paka eneo hili rangi uzipendazo.
3. Bandika mawingu katika sehemu ya anga karibu na picha ya Yesu.
4. Bandika mawe katika sehemu ya njia.
5. Mwishowe bandika shina za mti na sehemu za juu za mti ili kuweka miti katika sehemu ya njia.

Iko tayari. Unaweza kuiweka katika kirungu cha mlango au kuitundika ndani ya nyumba!

